




Kuku na Jongoo



Winy Asara ✎
Magriet Brink 🗣️
Matteo E. Mwitā 📄
Kiswahili 😊
Level 3 📖

(imageless edition)




Storybooks Canada

storybookscanada.ca


Kuku na Jongoo

Written by: Winy Asara
Illustrated by: Magriet Brink
Translated by: Matteo E. Mwitā

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Kuku na Jongoo walikuwa marafiki. Ila walikuwa wanashindana kila mara. Siku moja wakaamua kucheza mpira wa miguu ili waweze kubaini nani alikuwa mchezaji bora zaidi.

Wakaenda uwanjani na wakaanza
kucheza. Kuku alikuwa na kasi ila Jongoo
alikuwa na kasi zaidi. Kuku alipiga mpira
mbali, ila Jongoo alipiga mbali zaidi. Kuku
akaanza kupandwa na hasira.







Wakaamua kupigiana penati. Jongoo akaenda golini. Kuku alifunga goli moja pekee. Ikawa zamu ya kuku kwenda golini.



Tangu hapo, Kuku na Jongoo ni maadui.




Jongoo alipiga mpira akafunga. Jongoo
akapiga chenga akafunga. Jongoo akapiga
kichwa akafunga. Jongoo akafunga magoli
matano.




Kuku alikohoa, hadi akamtema jongoo
aliyekuwa tumboni mwake. Mama jongoo
na mwanaye wakakwea mti kujificha.




Kuku akakasirika kwa kuwa amefungwa. Hakuwa mshindani mzuri. Jongoo akaanza kucheka kwa sababu rafiki yake alikuwa analalamika.



Kuku akabeuwa. Akameza mate na kutema. Halafu akapiga chafya na kukohoa. Akakohoa tena. Jongoo alimfanya ajisikie vibaya.




kuku alipatwa na hasira kiasi kwamba
akafungua mdomo wake mkubwa na
akammeza Jongoo.



Mama Jongoo alipiga kelele, "Tumia nguvu
yako ya kipekee mwanangu!" Majongoo
wanaweza kutoa harufu mbaya na ladha
ya ajabu. Kuku akaanza kujisikia mgonjwa.



Kuku alipokuwa anarudi nyumbani alikutana na Mama yake Jongoo. Mama Jongoo akamuuliza, “Umemwona mwanangu?” Kuku hakujibu kitu. Mama Jongoo akapatwa na wasiwasi.



Mama Jongoo akasikia sauti kwa mbali. “Nisaidie mama!” ile sauti ililia. Mama Jongoo akaangalia huku na kule na kusikiliza kwa makini. Sauti ilitokea tumboni mwa kuku.